

Mwongozo wa ubora wa maziwa

Umuhimu wa ubora wa maziwa

Hakuna kitakachorekebisha ubora wa maziwa yakiwa yamesha haribika kwa mfugaji. Kwahiyo utunzaji wa maziwa, usafi na kudhibiti ubora hauna budi kuzingatiwa katika hatua zote za mlolongo wa thamani ya maziwa.

Uzalishaji wa maziwa yenye ubora wa hali ya juu huanzia sehemu ya kukamulia, ambayo lazima iwe safi, kavu na yenye hewa ya kutosha. Ngombe anatakiwa kukamuliwa kwenye sakafu laini isiyoteleza (saruji ikiwezekana). Sakafu hii inatakiwa iwe na mteremko kidogo ili kutiririsha majimaji na taka nyingine..

Kanuni bora za ukamuaji

Maandalizi ya kukamua


- Safisha eneo la kukamulia
- Mkamuaji anatakiwa awe na afya njema na awe anaosha mikono yake kabla ya kukamua.
- Safisha vyombo vya kukamulia kwa kutumia mchanganyiko maalum wa dawa (ml 4 za dawa na lita 2 za maji).
- Kamua ng'ombe kwa muda maalum na sehemu ileile au moja kila siku.
- Wape ng'ombe nyasi kavu na safi, ambayo wanaweza kula wakati wa ukamuaji.
- Osha kiwele na kila chuchu kwa maji ya uvuguvugu kwa kutumia taulo aukitambaa safi cha pamba kwa kila ng'ombe..
- Tumia kitambaa/taulo safi na kavu kukaushia chuchu.
- Lainisha kiwele kwa kutumia mafuta maalum ya kukamulia.
- Anza kumkamua ng'ombe dakika mbili baada ya kukamilisha taratibu za kumhamasisha ng'ombe kutoa maziwa (mfano kuosha na kukausha kiwele, kulainisha chuchu).



Mfugaji humpa ng'ombe majani makavu kabla ya kukamua.

Wakati wa kukamua

- Mkamue Ng'ombe kwenye sehemu safi iliyotengwa kwa ajili hiyo.
- Tumia njia ya kuminya kukamua badala ya kuvuta chuchu.
- Chunguza maziwa ya kwanza ya kila chuchu kuangalia ugonjwa wa kiwele.
- Kamua kwenye chombo kisafi cha metali. Usitumie chombo cha plastiki.



Maziwa lazima yakusanywe kwenye vyombo safi vy bati.

Baada ya kukamua

- Chovya chuchu kwenye asilimia 0.5 ya madini joto yatakayopatikana.
- Chuja maziwa kwa kutumia chujio au kitambaa kisafi.
- Pima na kuandika kiasi cha maziwa kwenye kitabu cha kumbukumbu ya maziwa.
- Hifadhi maziwa kwenye chombo kisichopata kutu au chombo cha bati.
- Safirisha maziwa kwa wasindikaji ndani ya saa moja baada ya kukamua.



Kudhibiti ugonjwa wa kiwele

Ng'ombe wasio na afya njema hula kidogo na huzalisha maziwa kidogo ambayo hayana ubora. Utunzaji wa ng'ombe mwenye afya ni muhimu.

Ugonjwa ambao mara nyingi huwapata ng'ombe ni kuvimba ugonjwa wa kiwele. Kuvimba Ugonjwa wa kiwele hutokana nani maambukizi yakatika kiwele ambayo yanaweza kuathiri haribu tishu za kuzalishia maziwa. Uharibifu huu unaweza kusababisha hasara ya uzalishaji kwa asilimia 15 au zaidi kwa ngombe mmoja. Huu ukosefu wa maziwa, pamoja na ukijumlisha na gharama za huduma ya utunzaji mifugo, unaweza kusababisha hasara kubwa ya kiuchumi kwa mfugaji.

Kuvimba Ugonjwa wa kiwele kwa ujumla kuna dalili zenye kutambulika kirahisi; maziwa huonekana kuwa na michirizinyuzi/chembechembe na huonyesha



Mazingira safi husaidia kupunguza ugonjwa wa kuvimba kiwele

dalili za kubadilika rangi kuwa uwekundu na unjano usio wa kawaida na kuganda. WakatiNyakati nyinginemwingine, huwa hamna dalili zinazoonekana. Ng'; Ng'ombe wenye ugonjwa wa kuvimba kiwele wanatakiwa kukamuliwa mwishoni, na maziwa yatakyokamuliwa yamwagwe.

Mazingira safi husaidia kupunguza ugonjwa wa kuvimba kiwele

Vimelea katika mazingira

Aina hii ya vimelea hupatikana kwenye mazingira ya ng'ombe. (mfano wanapolala, kwenye mbolea na tope), na maambukizi mengi hutokea ndani ya siku 75 za mwanzo za kunyonyesha. Ili kuzuia ugonjwa huu, wafugaji hutakiwa kuweka mazingira safi na makavu kwa ajili ya ng'ombe. Matumizi ya dawa aina ya iodine katika kuosha chuchu za ng'ombe husaidia pia, kama ilivyo kwa chakula bora chenye vitamini na madini.

Maambukizi ya Vimelea

Maambukizi ya bakteria vimelea huweza hutokea kutoka kwa ngombe mmoja kwenda kwa mwingine. Njia yenye maambukizi sana kutoka kwa ng'ombe aliyeathirika kwenda kwa ng'ombe mwenye afya ni kugusa (contagious) hasa kupitia mikono ya mkamuaji wakati wa kukamua. Aina hii ya kuvimba kiwele kinachosamba amaambukizi hudhibitiwa



Programu ya Maendeleo shirika la Land O'Lakes ni kuwezesha ukuaji wa kiuchumi, kuboresha afya na lishe, na kupunguza umaskini kwa kuwezesha mbinu kabambe za kukuza biashara zinazokidhi mahitaji ya soko katika;

- Uzalishaji wa kilimo wenye tija na ushindani
- Uendelezaji Biashara na ushirika
- Mifumo ya chakula na usalama kwa walaji
- Usalama wa chakula na hali ya maisha
- Lishe na Afya

Tanzania: Kitalu Na.79 corridor Area II, Mtaa wa Kiltex S.L.P 10106, Arusha, Tanzania; simu; +255 27 254 8530

Tovuti: www.idd.landolakes.com